SHULE YA SEKONDARI MWANZOLI

S.L.P 401,

NZEGA.

TAREHE ……

Kumb Na …….

Jina la Mwanafunzi ……..

S.L.P……

YAH: <u>MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MWANZOLI HALMASHAURI YA NZEGA MJI, MKOA WA TABORA - MWAKA 2021</u>

1.0 <u>UTANGULIZI</u>

Ninafuraha kukupongeza na kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika SHULE YA SEKONDARI YA MWANZOLI mwaka **2021,** Shule hii ipo umbali wa km 15 mashariki mwa Halmashauri ya mji wa Nzega.

Muhula wa masomo unaanza tarehe **…11../….01./2021** na unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **…11…/…01…/2020** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **..…18./…01…/2021 ndani ya siku saba tu.**

2.0 <u>MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA</u>

2.1 <u>SARE YA SHULE</u>

a) **Wavulana** ni SURUALI ZA BLUE BAHARI (2) MBILI pamoja na tai rangi ya kitambaa cha suruali na mkanda mweusi wa ngozi. Aidha mshono wa suruali ni lazima iwe na malinda mawili kushoto na malinda mawili kulia na pindo la chini ni turn up. Haturuhusu suruali za kubana na zisizofuata maelekezo ya hapo juu.

b) **Wasichana** ni SKETI MBILI ZA BLUE BAHARI pamoja na tai rangi ya kitambaa cha sketi. Maelezo ya mshono wa sketi ni linda box kubwa mbele na nyuma na malinda madogo mawili kushoto na malinda madogo mawili kulia pia sketi iwe ndefu yenye staha. **Kwa wasichana wa kiislamu wanaruhusiwa kuvaa hijab nyeupe kitambaa aina ya haluwa.**

c) Shati mbili nyeupe za mikono mifupi kwa wasichana na wavulana.

d) **Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba na visigino vifupi, haturuhusu viatu vingine vyenye marembo marembo au Raba kwa wavulana na wasichana pia.**

e) Soksi nyeupe jozi mbili wasichana na wavulana.

f) T-shirt moja RANGI LIGHT BLUE yenye nembo ya shule.

g) Sweta la LIGHT BLUE

2.2 <u>SARE ZA MICHEZO</u>

a) BUKTA YA BLUU moja kwa wavulana.

b) TRACK SUTI YA BLUU moja kwa wasichana.

2.3 <u>VIFAA VYA USAFI WA MAZINGIRA</u>

Ili kufanikisha suala la usafi hapa shuleni mwanafunzi anaporiti anapaswa aje na vifaa vya kufanyia usafi kama ifuatavyo:-

a) Jembe moja lenye mpini

b) Fyekeo moja

c) Fagio la nje (chelewa) moja

d) Ndoo ndogo, fagio la ndani au reki (ataleta kimoja tu kati ya hivi baada ya kupewa maelekezo).

2.4 MAHITAJI MENGINE MUHIMU

Mahitaji hayo ni pamoja na madaftari 12 (counter books), kalamu, penseli, mathematical set, vitabu, kamusi, file (spiral file). picha za rangi (passport size 3) pamoja na nakala ya cheti cha kuzaliwa.

2.5 USAFI WA MTU BINAFSI

Ni lazima mwanafunzi awe safi na nadhifu, ***Anyoe Nywele ziwe fupi zisizo na mtindo wowote***. Kucha ni lazima ziwe fupi na bila rangi. Sare ziwe safi na ziwe zimenyooshwa, viatu viwe na hali nzuri na vipigwe kiwi. **NB: Shule hairuhusu kusuka kwa wanafunzi wa kike.**

2.6 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi, yenye dhamana ya Elimu chini ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

a) Heshima kwa viongozi, Wazazi, Wafanyakazi wote, Wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (Preparation).
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na;
i) Kutunza mali za shule.

2.7 MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

1. Wizi
2. Uasherati, Ubakaji, Ushoga na Ulawiti
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya, biashara ya madawa yoyote ya kulevya
4. Makosa ya jinai
5. Kupigana au kupiga mwanafunzi mwenzake, mwalimu au mtumishi asiye mwalimu
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma na ya watu wengine
7. Kudharau bendera na wimbo wa Taifa
8. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule Kutoa au kushawishi kutoa mimba
9. Kuoa au Kuolewa
10. Kugoma, kuchochea na kuongoza migomo au kuvuruga amani na usalama wa watu shuleni
11. Kukataa adhabu iliyotolewa na mwalimu
12. Utoro (kutohudhuria shule bila taarifa kwa zaidi ya siku **90)**
13. Kukataa kufanya mazoezi na mitihani shuleni
14. Kumiliki au kuwa na SIMU ya mkononi
15. Kutembelea nyumba za kulala wageni, kumbi za starehe, baa, klabu na sehemu zingine ambazo kisheria mwanafunzi haruhusiwi.
16. ya kusoma taratibu zote za shule hii na kuzielewa

2.8 FOMU NA 1. UTHIBITISHO WA KUJIUNGA NA SHULE

A. TAMKO LA MWANAFUNZI:

Mimi …… nimezisoma na kuzielewa sheria za shule na ninaahidi kwamba nitazingatia na kutii masharti, sheria za shule na maelekezo mengine nitakayopewa na Walimu na Viongozi wote wa Shule, nikikiuka sheria hizo, hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi yangu kwa mujibu wa kanuni, taratibu na sheria zilizopo.

Tarehe: …… Saini: ……..……..…

B. TAMKO LA MZAZI LA KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

Mimi…….. ambaye ni Mzazi/Mlezi, nimesoma / nimesomewa sheria na maagizo mengine ya shule yanayomhusu mwanafunzi ……..…… na ninaahidi kutimiza wajibu wangu nikiwa Mzazi/Mlezi wa mtoto huyu kwa kumshauri ipasavyo pamoja na kumtimizia mahitaji yake ya shule.

Jina la Mzazi/Mlezi …….……. Sahihi …….

Tarehe…… Namba ya simu…….……..……..…….

MWISHO:

Natumia nafasi hii kukukaribisha **Shule ya Sekondari Mwanzoli** na ni matarajio yangu kuwa utaitumia vyema nafasi hii uliyopewa na Taifa lako.

……

EMANUEL G. WILSON

KAIMU MKUU WA SHULE

KARIBU SANA MWANZOLI SEKONDARI

F: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

PART A:

To The Medical Officer,

…..……..……..……..

…..……..……

……..…….. (Name in full)

Please examine the above named student as to her /his physical and mental fitness for a full time student. The examination should include the following categories (i-x).

(i) Eyesight (ii) Hearing (iii) Speech (iv) Limbs (v) Venereal diseases (vi) Leprosy (vii) Epilepsy (Viii) Neurosis (ix) other serious diseases e.g. Asthma, T.B. etc. (x) Pregnancy for girls only.

Name ……..……..…… Date ……..…… Signature …….……...

PART B:

MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by a Government Medical Officer). I have examined the above named student and consider that he is fit/unfit for full time studies.

a) Eyesight…….…

b) Hearing…….....……

c) Speech……

d) Limbs……..…

e) Veneraldisease……..……

f) Leprosy……..…

g) Epilepsy…….

h) Neurosis……..……..

i) Other serious diseases e.gAsthma: ……..…….

j) Tuberclosis (TB)……

k) Pregnancy for girls only……

Other Comments:

……..……..…..

Name …….……..…… Date ……..…… Signature …….……...

STATION ……. DESIGNATION …….

N.B. I request this form to be returned to the school in a sealed envelope.